**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

**KUMB NA.HA.15/128/01/33** 13 FEBRUARI, 2026

# TANGAZO LA NAFASI ZA KUJITOLEA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa anawatangazia wananchi wote wenye sifa za kimuundo kutuma maombi ya kujitolea kwa nafasi iliyoainishwa hapa chini;

## 1.0 DEREVA DARAJA II - NAFASI 9

### 1.1. MAJUKUMU YA DEREVA DARAJA LA II

i) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
iii) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali pale inapohitajika
v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
vi) Kufanya usafi wa gari na
vii) Kazi nyingine atazopangiwa na Mwajiri.

### 1.1.1. SIFA ZA MWOMBAJI

i) Awe amehitimu kidato cha Nne (IV) au kidato cha Sita (VI).
ii) Awe mwenye Leseni ya udereva daraja "E au C1" ya uendeshaji pamoja na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
iii) Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
iv) Waombaji wenye Cheti cha majaribio ya ufundi daraja la II watafikiriwa kwanza.

### 1.1.2. MALIPO

Nafasi hizo zinalenga kuwapa wahitimu fursa ya kujifunza na kupata uzoefu na sio Ajira za kudumu. Watakaopata nafasi watalipwa posho kulingana na miongozo ya Serikali.

## 2.0. MASHARTI YA JUMLA.

I. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 35;

II. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua pepe (E-mail address) pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika;

III. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma Pamoja na cheti cha kuzaliwa vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili, Nakala ya kitambulisho cha Taifa au Hati ya kusafiria na picha mbili (2) ndogo za rangi.

IV. "Testimonial", "Provisioinal Result","Statement of result", hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita **(FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**

V. Waombaji watakao wasilisha taarifa za kughusi, watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria za Nchi.

VI. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 27 Februari, 2026

VII. Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:-

**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA,**
**15 BARABARA YA BOMA,**
**S. L. P 51,**
**65682 RUANGWA, LINDI.**

VIII. Maombi yatumwe kwa anuani tajwa hapo juu.

IX. Kujitolea hakutatumika kama sharti la kujipatia ajira ya kudumu isipokuwa kuwawezesha wahitimu kuendelea kujifunza na kupata uzoefu.

Tangazo hili Imetolewa na

ERNEST GEORGE HAULE
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

EXECUTIVE DIRECTOR
DISTRICT COUNCIL
RUANGWA
P.O. Box 51, RUANGWA